

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

638

VIELELEZO NA TEKNOLOJIA

Muda: Saa 3

Jumatatu, 13 Mei 2013 asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B.
2. Jibu maswali **yote** kutoka katika sehemu A na maswali **manne (4)** kutoka katika sehemu B.
3. Soma kwa makini maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya wino wa bluu au mweusi isipokuwa michoro ambayo itachorwa kwa penseli.
5. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Eleza kwa kifupi maana ya maneno yafuatayo kama yanavyotumika katika somo la Vielelezo na Teknolojia.
(a) Media (c) Metali
(b) Projekta (d) Modeli
2. (a) Eleza kwa kifupi dhana ya vielelezo na teknolojia.
(b) Bainisha aina tatu za vielelezo na teknolojia zinazotumika katika kufundisha na kujifunza.
3. Eleza kwa kifupi mbinu nne zinazoweza kutumika katika kufaragua na kutengeneza zana za kufundisha na kujifunza.
4. Eleza kwa kifupi vyanzo vinne vya zana za kufundishia na kujifunzia.
5. Eleza aina kuu mbili za vielelezo na teknolojia zinazotumika wakati wa kufundisha na kujifunza.
6. Toa sababu nne kuthibitisha ulazima wa walimu kutumia zana za kufundishia wakati wa mchakato wa kufundisha na kujifunza.
7. Bainisha mambo manne ya kuzingatia wakati wa kuchora mchoro kama zana ya kufundishia darasani.
8. Ifuatayo ni orodha ya vielelezo na teknolojia ambavyo vinatumika kufundishia na kujifunzia. Vipange katika makundi ya “vielelezo masikizi” na “vielelezo maono”.
Orodha
Vitabu/majarida na magazeti, sinema mnato, modeli ya mfumo wa mifupa, michoro, televisheni, vitu halisi, redio, picha mnato, ramani, video, simu na kanda ya kusikiliza.
9. Eleza kwa kifupi faida mbili na hasara mbili za matumizi ya vielelezo na teknolojia kisasa katika kufundisha na kujifunza.
10. Fafanua njia nne kuonesha namna kompyuta inavyoweza kutumika katika mchakato wa kujifunza na kufundisha.

SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **manne (4)** kutoka katika sehemu hii.

11. Toa hoja tano kuthibitisha usemi kwamba matumizi ya vielelezo huimarisha uwezo wa kukumbuka mambo aliyojifunza mwanafunzi.
12. "Matumizi ya vielelezo wakati wa mchakato wa kujifunza na kufundisha ni matumizi mabaya ya muda". Kanusha usemi huu kwa kutoa sababu zisizopungua tano.
13. Eleza changamoto tano anazoweza kukumbana nazo mwalimu wakati wa kufaragua na kutengeneza zana kwa ajili ya kufundishia na kujifunzia.
14. Eleza mambo matano kuonesha umuhimu wa machapisho katika kufanikisha mchakato wa kufundisha na kujifunza.
15. Eleza hatua tano za kuzingatia wakati wa kutumia tovuti kama chanzo cha taarifa wakati wa kufundisha na kujifunza.
16. Elezea makundi matatu ya vielelezo na teknolojia kisha toa mfano mmoja kwa kila kundi kudhihirisha matumizi yake darasani.
17. Tathmini umuhimu wa kutumia zana za aina mbalimbali katika kipindi kimoja.
18. Eleza ukitoa mifano mitano namna ambavyo vielelezo na teknolojia kisasa vinavyoweza kutumika katika shule za kitanzania.